

CHS katika lugha rahisi

Toleo halisi la Kiingereza la ahadi tisa za CHS liliotumiwa kama msingi wa tafsiri hii lilifanuliwa na Kikundi tenda- kazi pamoja na wataalamu wa Translators without Borders. Toleo la lugha rahisi la CHS linalenga kutumia maneno yanayotumika katika mazungumzo ya kila siku. Pia, linatumia miundo ya sentensi na maumbo ya vitenzi vinavyowezesha kuelewa kwa usahihi na kwa haraka.

Nia asili ya nyaraka hii ni kutoa taarifa kuhusu ahadi za mashirika ya kibinadamu katika njia inayoweza kueleweka na jamii na watu binafsi walioadhirika na janga.

Unaweza kupata yafuatayo kutoka katika shirika letu, kama mtu aliyeathiriwa na janga

Wakati shirika letu linapofanya kazi na jamii ili kuwasaidia kukabiliana na janga, tunaahidi kufuata ahadi jumla tisa. Ukurasa huu unaelezea ahadi hizo katika lugha rahisi, ili uweze kuelewa ni nini unatarajia kutoka kwetu.

Dharura zinaweza kusababisha matatizo kwetu pia. Hivyo ingawa muda wote tunajaribu kufuata ahadi hizi, muda mwingine tunaweza kushindwa kufanya hivyo. Lakini tunataka kujifunza ili tuweze kujiboresha, hivyo unaweza kutusaidia kwa kutupa maoni.

Tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kuhakikisha...

1. tunaelewa na tunatimiza mahitaji yako.
2. tunakupa msaada pale unapouhitaji.
3. tutakupa msaada utakaokuwezesha kurudi kwenye hali ya kawaida na kukuandaa kukabiliana na dharura kama hii kama itatokea tena. Hatutakudhuru.
4. tutakujulisha ni msaada gani unaweza kutarajia na ni kwa namna gani unatakiwa kushughulikiwa. Tutajaribu kadri ya uwezo wetu kukupatia nafasi ya kutoa maoni katika maamuzi kuhusu usaidizi/msaada unaopewa .
5. tutahakikisha kuwa unaweza kutoa taarifa kama hujaridhika na msaada tunaotoa au jinsi wafanyakazi wetu walivyokuhudumia. Hakuna atakayekudhuru kwa kuripoti malalamiko. Tutachukua hatua Kushughulikia malalamishi uliyowasilisha.
6. tutafanya kazi pamoja na mashirika mengine yanayotoa misaada. Tutajitahidi kuunganisha maarifa na rasilimali tulizonazo ili kutimiza mahitaji yako kwa ubora zaidi.
7. tutajifunza kutokana na uzoefu ili msaada tunaotoa uendelee kuboreka kadri muda unavyoenda.
8. tutahakikisha kuwa wafanyakazi wetu wana ustadi na uzoefu wa kukuhudumia.
9. tutasimamia rasilimali zetu kwa uangalifu, kuzuia ubadhirifu na kuhakikisha unafaidika zaidi.

Kumbuka: "rasilimali" inajumuisha vitu vyote, kama nyenzo, fedha, na huduma za afya, tunavyotumia kusaidia watu waliokumbwa na dharura.